

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA.

MKOA: NJOMBE

Simu : +255 - 26 2790120
Nukushi : +255 - 26 2790128
Barua pepe : ded@ludewadc.go.tz
Tovuti : ww.ludewadc.go.tz



MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S. L. P 19,
LUDEWA.

11/06/2020.

TANGAZO

YAH: TANGAZO LA ZABUNI YA KUUZA MITI.

1. Halmashauri inakaribisha Mashirika, Watu binafsi kununua miti iliyopo katika Shamba la miti la Halmashauri lililopo katika kijiji cha Madindo..
2. Miti inayouzwa ni aina ya Mipaina ipatayo 601 yenye ujazo (dbh) wa kuanzia sm 10 hadi sm 39 . Idadi ya miti iliyopo na ujazo wake ni kama ilivyo katika jedwali hapo chini :-

| Na | Diameter Size (SM) | Idadi ya miti |
|-------|--------------------|---------------|
| 1 | 10 - 28 | 486 |
| 2 | 29 - 38 | 110 |
| 3 | 39 - | 5 |
| JUMLA | | 601 |

3. Kwa wanaohitaji kununua watume barua za maombi kwa anuani ifuatayo **Katibu Bodi ya Zabuni S.L.P. 19 Ludewa** na juu ya bahasha iandikwe **ZABUNI YA KUNUNUA MITI**.
4. Mwombaji katika barua yake ya maombi anatakiwa kutaja kiasi cha fedha atakazolipa kwa miti yote 601 na mwombaji atakayeshinda ni yule atakayetaja bei ya juu zaidi ya waombaji wengine.
5. Waombaji wanaruhusiwa kuikagua miti husika iliyopo katika shamba la miti katika kijiji cha Madindo kwa siku za kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 09:30 alasiri. Mwombaji anatakiwa kumuona **Mtendaji wa Kata ya Ludende** kwa ajili ya kuoneshwa miti husika.
6. Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 24/06/2020 jumatano saa 4:00 asubuhi na ufunguzi utafanyika tarehe 24/06/2020 jumatano saa 04:30 asubuhi katika Ukumbi wa Halmashauri. Waombaji au wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria.


Sunday N Deogratius
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
LUDEWA.

Mkurugenzi Mtendaji
Miti ya Wilaya